



SIMU: +255-23-264 0034  
NUKUSHI: +255-23-264 0035  
BARUA PEPE: info@tosci.go.tz  
WAVUTI: www.tosci.go.tz

MAKAO MAKUU:  
S.L.P. 1056  
MOROGORO  
TANZANIA

Kumb. Na.: AB. 136/441/01/36

20/10/2023

Kwa: **Wafanyabiashara ya Mbegu,**  
**Tanzania Bara.**

**YAH: TAARIFA KUHUSU BEI ELEKEZI ZA MBEGU ZA MAHINDI ZINAZOUZWA KWA WAKULIMA**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Kama mtakavyokumbuka, tarehe 15 Oktoba 2023 Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein M. Bashe akiwa kwenye mkutano wa hadhara katika ziara ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mkoani Manyara, alitoa maelekezo kwa TOSCI kutangaza bei elekezi ya mbegu za mahindi kufuatia malalamiko ya wananchi kuwa wamekuwa wakiuziwa mbegu hizo kwa bei ya juu na bei hizo zimekuwa zikibadilika mara kwa mara.
3. Baada ya kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo uwezo wa wakulima kununua mbegu na gharama za makampuni kuzalisha au kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi, Waziri wa Kilimo ameelekeza bei elekezi iwe kama ifuatavyo:

**Bei elekezi kwa mbegu za mahindi**

Bei elekezi ya mbegu za mahindi kwa msimu wa kilimo wa 2023/2024 itakuwa kama ifuatavyo:

- i. **Aina za mbegu zinazochavushwa huria (Open Pollinated Varieties – OPVs)**  
Bei elekezi kwa mbegu za aina zinazochavushwa huria itakuwa **4,000/=** kwa kilo moja au **8,000/=** kwa kifungashio cha kilo mbili.
- ii. **Aina za mbegu chotara (Hybrid Varieties), zinazokomaa mapema na muda wa kati**  
Bei elekezi kwa mbegu za aina chotara zinazokomaa mapema au muda wa kati itakuwa **7,150/=** kwa kilo moja au **14,300/=** kwa kifungashio cha kilo mbili.

- iii. **Aina za mbegu chotara (Hybrid Varieties), zinazokomaa kwa muda mrefu**  
Bei elekezi kwa mbegu za aina chotara zinazokomaa kwa muda mrefu itakuwa **8,000/=** kwa kilo moja au **16,000/=** kwa kifungashio cha kilo mbili.
- iv. Bei elekezi za mbegu chotara zinazokomaa kwa muda mfupi na zinazokomaa kwa muda mrefu zinatofautiana kutokana na gharama kubwa inayotumika kupata mbegu za vizazi kwa ajili ya uzalishaji wa aina ya mbegu chotara zinazokomaa kwa muda mrefu.
4. Ili kuhakikisha kuwa wakulima wanauziwa mbegu kwa bei isiyozidi viwango elekezi, Waziri ameyataka makampuni kuwaelekeza mawakala wao wanaowauzia wakulima kutokuuza mbegu kwa zaidi ya bei elekezi na pia ameelekeza kuwa vyombo vya Serikali vitahakikisha mwongozo huu unazingatiwa kikamilifu.

**Bei elekezi kwa mbegu za mazao mengine**

Bei elekezi ya mbegu za mazao mengine zitaendelea kutolewa kadiri mahitaji yatakavyojitokeza.

5. Nawatakia utekelezaji mwema na ninawashukuru kwa ushirikiano wenu.

Patrick Ngwediagi  
**MKURUGENZI MKUU**

Nakala:

Katibu Mkuu,  
Wizara ya Kilimo,  
Mji wa Serikali Mtumba,  
**DODOMA**

Mkurugenzi Mtendaji,  
TASTA,  
**ARUSHA.**